UMUHIMU NA FADHILA ZA KUHIFADHI QUR-AN

Ni jambo bora kiasi gani kuhifadhi maneno ya Allah, muumba wa kila kitu. Kiufupi, tutataja baadhi ya aya na hadithi za Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi Wasallam) juu ya umuhimu na fadhila za kuhifadhi qurani.

Aya 1

Anasema Allah aliyetukuka katika kitabu chake.

“Bali hizo ni aya zilizo wazi katika vifua vya waliopewa elimu”
(‘Ankabut: 49).

Mtu aliyehifadhi quran katika kifua chake basi amebeba elimu kubwa mno hamna mfano wake.

Hadithi 1

Kutoka kwa ‘Abdullah ibn ‘Umar (Allah awaridhie yeye na baba yake) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

***“Ataambiwa mtu wa quran, soma na panda daraja za peponi na soma kama ulivyokuwa ukiisoma katika dunia, kwa hakika daraja lako la peponi ni mpaka aya yako ya mwisho utakayoisoma* (kwa kuhifadhi)”**

(Abuu Daawud: 1464 na at-tirmidhiy: 2914)

Amesema Sheikh Albaniy (Allah amraham)
“Tambua kwamba “Swahibu wa quran” ni mwenye kuihifadhi moyoni [Silsilatul – ahaadith Asw-swahiyhah (5/284)]

Bila ya shaka, pepo ina daraja kama alivyosema Allah katika kitabu chake ila kwa mujibu wa hadithi hii daraja la aliyehifadhi qurani huko peponi ni daraja la juu. Anasema Allah aliyetukuka.

***“Na viumbe wote watakuwa katika daraja zao mbalimbali kwa yale waliyoyatenda”* (Ahqaaf: 19)**

Hadithi 2

Kutoka kwa Anas ibnu Maalik amesema kuwa amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Kwahakika Allah ana watu wake wa karibu miongoni mwa wanadamu wakasema (maswahaba kumuuliza Mtume wa Allah) ewe Mtume wa Allah, kina nani hao? Akasema “ni watu wa quran, hao ndio watu wa Allah na amewachagua” (Ibnu majah: 215)

Hadithi 3

Kutoka kwa Abuu Huraira (Allah amridhie) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Kwa hakika ipo sura katika quran ina aya thelathini itamuombea msamaha mtu wake mpaka atasamehewa nayo ni tabaarakalladhiy biyadihil mulku”
(Abuu Dawuud:1400 na attirmidhiy:284)

Sura hii humuombea msamaha mtu wake kaburini na ndio maana kabla ya kulala kila siku Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) alikuwa akiisoma na akisema sura hiyo ni kinga dhidi ya adhabu ya kaburi.

Hadithi 4

Kutoka kwa Abuu Umaamah amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Isomeni quran, kwa hakika itakuja siku ya qiyaamah ni yenye kuwaombea msamaha watu wake.” (Muslim: 804)

Hadithi 5

Kutoka kwa ‘Uqbata ibn ‘Aamir amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Lau kama quran itawekwa katika ngozi kisha ikatupwa motoni haitaungua”
(Ahmad: 17365 na Daarimiy: 3353 na ameisahihisha Sheikh Albaaniy kwa daraja la hasan)

Vipi kwa mtu aliyehifadhi quran?! Quran itakuwa ni sababu ya Allah kumkinga na adhabu ya kuungua katika moto wa jahannam.
Wamekhtilafiana wanachuoni juu ya hadithi hii. Kuna waliosema ikiwa qurani itawekwa katika ngozi kisha ikatupwa motoni basi itaungua ngozi na wino wake lakini quran haitaungua kwani Allah atainyanyua kwakuwa ameahidi ataihifadhi. Kuna wengine waliosema hapa anakusudiwa yule ambaye Allah amemchagua kwa kuhifadhi quran kifuani kwake, Allah atamkinga na adhabu ya kuungua katika moto wa jahannam. Yaani, ikiwa aliyehifadhi qur-an ataingia katika moto wa jahannam basi hatoungua.

Aidha, mtu aliyehifadhi quran hutangulizwa katika mambo mengi kama yalivyokuja katika hadithi mfano: hutangulizwa katika mwanandani kama tunataka kuwazika watu wawili pamoja, hutangulizwa katika kuwaongoza watu katika swala na pia hutangulizwa katika kupewa mke na kadhalika.

Hadithi 6

Kutoka kwa Jaabir ibn Abdillah (Allah awaridhie yeye na baba yake) amesema.

"Alikuwa Mtume (Swalla Allahu 'alaihi wasallam) anawakusanya watu wawili waliokufa katika vita vya uhud katika sanda moja (wakati wa kuwazika) kisha anasema "nani katika hawa amehifadhi sana quran?" atakapoashiriwa (kuwa ni fulani) basi humtanguliza katika kaburi" (Bukhariy: 1278).

Hii ni kuonyesha namna ambavyo Mtume Swalla Allahu 'alaihi wasallam alivyokuwa akiwathamini sana waliohifadhi qurani mpaka wakati wa kuwazika.

Hadithi 7

Kutoka kwa Sahli ibn Sa'd (Allah amridhie) amesema

"Alikuja mwanamke mmoja mpaka kwa Mtume (Swalla Allahu 'alaihi wasallam) akasema "ewe Mtume wa Allah, nimekuja kukupa nafsi yangu ili unioe" akasema mtu mmoja (aliye karibu) "niozeshe mimi" akasema Mtume (Swalla Allahu 'alaihi wasallam) "Tumeshakuozesha kwa kile ulichokuwa nacho katika quran" (Bukhariy: 2310).

Katika riwaya nyingine imekuja, swahaba alipomwambia Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) ***“ewe Mtume wa Allah, ikiwa huna haja nae, niozeshe mimi” Akasema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) “Una kiasi gani cha quran?” Akajibu “sura fulani na sura fulani akazihesabu, Akasema “Unazisoma kwa moyo wako (umezihifadhi)? Akajibu “ndio”***
Akasema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) “Nenda, nimekuozesha kwa quran uliyoihifadhi” (Bukhariy: 5871)
Hadithi hii ni “muttafaqun ‘alaihi” na imekuja katika lafdhi nyingine kiurefu zaidi. Kwa ufupi hadithi hii inaonyesha namna Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) alivyokuwa akiithamini quran mpaka kufikia kumpa swahaba mke kwa ile quran aliyoihifadhi.

Hadithi 8

Kutoka kwa ‘Aisha (Allah amridhie) amesema kuwa amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Hodari wa quran yupo pamoja na malaika waandishi, watukufu walio watiifu na yule ambaye anasoma quran na anakwamakwama kwa kupata uzito hali ya kuwa anafanya jitihada basi ana ujira mara mbili” (ujira wa kupata tabu kwa ajili ya Allah na ujira wa kisomo cha quran kwa kila herufi pasina kumzidi yule wa mwanzo)” (Muslim: 798)

Amesema Imamu An-nawawiy katika “al-minhaaj” katika “tafsir Swahih Muslim” na Imamu ibnu Hajar katika “fat-hul baariy” katika “tafsir swahihil bukhariy” kusherehesha hadithi hii kuwa hodari wa quran ni aliyehifadhi quran vizuri kwa ubora wa kiwango.

Katika lafdhi nyingine ya imamul Bukhariy.

“Mfano wa yule ambaye anasoma quran hali ya kuwa ameihifadhi basi yupo pamoja na malaika waandishi watukufu walio watiifu. (Bukhariy: 4937)

Ni cheo kikubwa kiasi gani hiki!!! Kwamba aliyehifadhi quran yupo pamoja na malaika waandishi, watukufu na watiifu kila atakapokuwa. Bishara njema kwa waliohifadhi qurani. Vipi utajisikia ewe uliyehifadhi qurani utakapokutana na mola wako hali ya kuwa una maneno yake kifuani mwako?!

Hadithi 9

Mtu aliyehifadhi qur-an na akawa anaisoma hiyo qur;an nyakati za mchana na nyakati za usiku ni mtu wa kumuonea wivu sana.

Kutoka kwa ‘Abdillahi ibn ‘Umar (Allah amridhie) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wassallam)

“Hakuna husda (wivu) isipokuwa kwa mambo mawili, mtu ambaye Allah amempa qur-an akawa anaisoma nyakati za usiku na nyakati za mchana, na mtu ambaye Allah amempa mali akawa anaitoa mali hio nyakati za usiku na nyakati za mchana” (Bukhariy: 7529)

Hawa ni watu wa kuwaonea sana wivu, Allah atupe kama wao ili tufanye kama wao au zaidi yao.

Hadithi 10

Kutoka kwa Abuu Dardaai (Allah amridhie) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Atakayehifadhi aya kumi za mwanzo katika Suratul – Kahfi ataepushwa na fitna ya Masihi Ad-dajjal”
(Muslim: 809 na Abuu Daawud:4323)

Ikiwa kuhifadhi aya 10 tu katika Suratul Kahfi, mtu atapewa kinga hii na Allah kutokana na fitna kubwa ya Masihi Ad-dajjal, vipi yule ambaye amehifadhi msahafu mzima?!

Hadithi 11

Kumuheshimu na kumkirimu mtu aliyehifadhi qur-an ni katika kumtukuza Allah.

Kutoka kwa Abuu Musa (Allah amridhie) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Kwa hakika katika kumtukuza Allah ni kumkirimu mzee (kikongwe mwenye mvi) aliye muislamu, na aliyehifadhi qur-an ambaye hapituki mipaka wala kuipuuza hiyo qur’an na kumkirimu mtawala muadilifu”
(Abuu Daawud:4843)

Hadithi 12

Kutoka kwa Abuu Huraira (Allah amridhie) amesema kuwa, amesema Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam)

“Atakuja mtu wa qur-an siku ya qiyamah, basi qur-an itasema “ewe mola wangu mpambe huyu” basi atavalishwa taji la heshima, kisha itasema (qur-an) “ewe mola wangu mzidishie” basi atavalishwa vazi la heshima, kisha itasema (qur-an) “ewe mola wangu mridhie” basi Allah atamridhia”
(At tirmidhiy: 2915, Al-haakim: 2029 na Al-bazzaar:9035)

Hadithi 13

Kutoka kwa ‘Abdullah ibn Buraydah naye kutoka kwa baba yake (Allah awaridhie) amesema kuwa “Nilikuwa nimekaa na Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam), basi nikamsikia akisema;

“Jifunzeni suratul baqarah kwani kwa hakika kuichukua sura hiyo ni baraka na kuiacha ni majuto na wala hawaiwezi wachawi” kisha Mtume (Swalla Allahu ‘alaihi wasallam) akanyamaza kidogo kisha akasema:
“Jifunzeni suratul baqarah na suratu Aali- ‘imraan, kwani kwa hakika sura hizo mbili ni zenye kutoa mwangaza, na kwa hakika sura hizo mbili zitamfunika (zitamtengenezea kivuli) mtu wake siku ya qiyaamah kama vile ni viwingu viwili au makundi mawili ya ndege waliokunjua mbawa zao. Na kwa hakika qur-an itampokea mtu wake siku ya qiyaamah wakati litakapopasuka kaburi lake (akiwa na uchovu mkubwa) kama vile mtu mtu aliyebadilika rangi kutokana na maradhi au safari ndefu.
Basi qur-an itamwambia: “Je, unanijua mimi?”
Atajibu “sikujui” qur-an itamwambia:
“Mimi ni rafiki yako qur-an ambaye nilikutia kiu wakati wa joto kali mchana na nikakufanya ukeshe katika usiku wako (yaani nikakunyima usingizi).
Kwa hakika kila mfanyabiashara yupo nyuma ya biashara yake (anaifuatilia ili apate faida ya biashara yake). Na kwa hakika wewe leo upo nyuma ya biashara yako (yaani unatarajia faida ya ile qur-an). Basi atapewa ufalme kwa mkono wake wa kulia na maisha ya milele kwa mkono wake wa kushoto na atawekewa juu ya kichwa chake taji la heshima. Na watavishwa wazazi wake wawili mavazi mawili ya mapambo ambayo dunia yote haitoweza kununua mapambo hayo. Watasemaa (Wazazi wake wawili kwa furaha), “Kwanini tumevishwa mapambo haya?!” watajibiwa; “kwakuwa mtoto wenu alihifadhi qur-an.”
Kisha ataambiwa “soma na panda katika daraja za peponi na maghorofa yake.” Basi ataendelea kupanda daraja za peponi maadamu anasoma haraka haraka au taratibu”.
(Ad daarimiy: 3434, Ahmad: 22950 na Ibnu Majah:3781)

NAMNA RAHISI YA KUHIFADHI QURAN

Kuhifadhi qur'an sio jambo gumu ijapokuwa umri una nafasi fulani katika kuhifadhi quran. Mtoto mdogo au kijana mwenye umri mdogo anakuwa na hifdhi nzuri isiyotoka kiwepesi kuliko mtu mzima. Pia, aliyehifadhi quran kipindi alivyokuwa mdogo hata hifdhi yake ikipotea ni rahisi kuirudisha bila ya kutumia nguvu nyingi kuliko aliyehifadhi ukubwani. Hii ni kwasababu mwenye umri mdogo kichwa chake hakina mambo mengi na wala bado hajaanza kuandikiwa dhambi au madhambi yake ni machache sana ukilinganisha na mtu mzima mwenye mambo mengi kichwani na madhambi. Anasema Allah aliyetukuka.

"Na mcheni Allah na Allah atakupeni elimu" **(Baqarah: 282)**

Hii haimaanishi mtu mzima hawezi kuhifadhi quran, hapana mtu mwenye umri mkubwa anaweza kuhifadhi qurani na akawa na hifdhi nzuri tu ila akizembea kidogo tu inakuwa ni nyepesi zaidi kutoka kuliko yule ambaye amehifadhi quran katika umri mdogo. Qurani ni nyepesi kuihifadhi ndio maana Allah akasema katika kitabu chake.

"Kwa hakika tumeifanya qurani kuwa nyepesi ili iwe ni ukumbusho."
(Qamar: 17)

Ni muhimu sana wanafunzi wakaelekezwa na kupewa mbinu za namna ya kuhifadhi quran tukufu.

Nini ufanye ili uweze kuhifadhi quran tukufu kwa urahisi?

Mfano unataka kuhifadhi ukurasa wa mwanzo katika suratul – Mulku.

(1) Soma aya ya kwanza mara 15 au zaidi.
(2) Soma aya ya pili mara 15 au zaidi.
(3) Soma aya ya tatu mara 15 au zaidi.
(4) Endelea hivi kusoma kila aya moja mara 15 au zaidi, mpaka umalize ukurasa wote.
(5) Baada ya kumaliza kurudia aya mojamoja mara 15 au zaidi, soma ukurasa wote kuanzia mwanzo wa ukurasa mpaka mwisho wake mara 15 au zaidi. Utaona ukurasa huu ni mwepesi sana baada ya kufunga msahafu na kusoma bila kuangalia.
(6) Kwa utaratibu huu utahifadhi ukurasa mmoja kwa takriban dakika 30.

Muhimu kuzingatia

- Baadhi ya wanafunzi hurudia kila aya mara 15 au zaidi lakini wakati wanarudia ukurasa wote kuanzia aya ya mwanzo mpaka aya ya mwisho wa ukurasa huwa wavivu, kwa kurudia mara 3 au mara 4!!! Kufanya hivi ni makosa kwani hifdhi yako itakuwa dhaifu. Wakati unarudia mara nyingi ukurasa mzima ni muhimu mno kwani ndio kuhifadhi haswaa. Kwahiyo ni muhimu mno kurudia mara 15 au zaidi ili kuuzoesha ulimi kuwa ikitoka aya fulani inakuja aya fulani na sio kurudia ukurasa mara 3 au mara 4 inakuwa bado haujauzoesha ulimi mpangilio wa aya.
- Baadhi ya aya zinaweza kuwa ndefu, hivyo igawe aya katika sehemu mbili au tatu au zaidi, halafu kila kipande cha aya utarudia mara 15 au zaidi mpaka umalize ukurasa unaotaka kuhifadhi. Baada ya hapo utarudia kusoma ukurasa wote mara 15 au zaidi.
- Ukizidisha kurudia zaidi ya mara 15 ni bora zaidi kwani hifdhi yako inazidi kuwa bora zaidi.
- Ukitaka kuhifadhi zaidi ya ukurasa mmoja inapaswa ufanye hivi kwa kila ukurasa unaotaka kuhifadhi ila anayehifadhi nusu ukurasa atarudia kila aya mara 15 au zaidi kisha atasoma kuanzia mwanzo wa ukurasa mpaka katikati yake mara 15 au zaidi.

Mara ngapi utasoma kwa kuangalia katika msahafu na mara ngapi utasoma bila kuangalia wakati unahifadhi quran?

(1) Wakati unarudia kila aya mara 15 au zaidi, hakikisha mara nyingi unakuwa unaangalia katika msahafu mfano mara 10 kwa kuangalia na mara 5 bila kuangalia.

(2) Mwingine kila aya anarudia mara 20 hivyo mara 10 kwa kuangalia na mara 10 bila kuangalia. Kisha baada ya hapo anasoma ukurasa wote kuanzia mwanzo mpaka mwisho mara 20. Kila unavozidisha idadi ya kurudiarudia ndipo hifdhi yako inazidi kuwa kali zaidi.

Faida yake

(i) Unavyokuwa unaangalia katika msahafu wakati wa kuhifadhi, **macho** pia yanahifadhi ule mpangilio wa aya yaani unakuwa unahifadhi pia sura imeanzia wapi katika msahafu juu au katikati ya ukurasa na pia aya imeandikwaje, ipo katikati ya ukurasa au juu au chini ya ukurasa. Yote haya mtu aliyehifadhi quran anakuwa anajua aya fulani ipo juu ya ukurasa au katikati au chini ya ukurasa. Kwahiyo, wakati unarudiarudia aya mara 15 au zaidi ni vizuri mara nyingi ukawa unaangalia katika msahafu.

(ii) Lakini unavyokuwa unarudia kila aya mara nyingi hilo husaidia kuuzoesha **ulimi** aya hio na unavyokuwa unarudia ukurasa mzima mara nyingi hilo husaidia pia kuuzoesha ulimi kuwa ikitoka aya fulani inakuja aya fulani.

Muhimu kuzingatia

- Usihifadhi quran kwa kutumia spidi ndogo, tumia spidi ya katikati au spidi kubwa lakini herufi ziwe zinasikika kwani lengo ni kuuzoesha ulimi quran na mpangilio wake.
- Wakati wa kuhifadhi quran, toa sauti ni lazima usikie unachokihifadhi kwani hatuhifadhi qurani kimoyomoyo kama tunavyohifadhi masomo ya shuleni kama baiolojia.

Kama unataka kuhifadhi ukurasa mwingine siku inayofuata, nini ufanye?

Ikiwa unataka kuhifadhi ukurasa mpya siku inayofuata, kabla ya kuanza kuhifadhi kwa utaratibu tulioutaja hapo juu, soma kwanza ukurasa uliohifadhi jana mara 5 yaani mara 3 kwa kuangalia na mara 2 bila kuangalia. Kufanya hivi husaidia ulichokihifadhi kabla kukita katika kifua chako kabla ya kuongeza kingine kipya. Baada ya hapo endelea kuhifadhi ukurasa mwingine mpya kwa utaratibu uliotajwa hapo awali.

Namna gani unaweza kutofautisha aya zinazofanana katika quran wakati unapohifadhi?

Njia nzuri ni kwamba, wakati wa kuhifadhi utakapohisi aya unayohifadhi inafanana na aya nyingine katika sura nyingine, fungua msahafu kuziangalia aya hizo mbili kwa pamoja kisha angalia tofauti yake. Ukishabaini tofauti ya aya hizo mbili weka kanuni yako ya kukumbuka tofauti ya aya hizo mbili, kwahiyo, unakuwa unajua nikiwa nasoma aya hii nitapita hivi na nikiwa nasoma aya ile nitapita vile.

Mfano: Unahifadhi Suratul – muddathir ukakutana na aya inasema “Kallaa **innahuu** tadhkirah” ukahisi ipo aya kama hio katika sura nyingine ukakumbuka ni suratu ‘abasa fungua msahafu kuziangalia aya hizo mbili tofauti yake utakuta katika suratu ‘abasa ni “Kallaa **innahaa** tadhkirah”. Kwahiyo unaweka akilini tofauti hio na kama kuna uwezekano wa kuweka kanuni yako ya kukumbuka tofauti hio ni vizuri zaidi.

Mambo ya kuzingatia wakati unahifadhi quran.

(1) Ni vizuri kuhifadhi quran kuanzia suratun-naas mpaka suratul-baqarah kwasababu ni rahisi na baada ya kumaliza kuhifadhi quran muraja'a wako inabidi uanzie suratul-baqarah mpaka suratun-naas.

(2) Hakikisha unahifadhi quran na kusikilizwa na mwalimu ili apate kukusahihisha makosa yako kwa kila ukurasa. Kutofanya hivyo huenda ukauzoesha ulimi makosa na ikawa ngumu kuliondoa kosa hilo mpaka urudie rudie sana kwa usahihi wake. Tambua kuwa kosa ambalo uterekebishwa na mwalimu wako au mtu yeyote atakayekukumbusha wakati anakusikiliza au wakati unaswalisha swala ni vigumu kulirudia kosa hilo siku nyingine kwani utakuwa tayari umeshazingatia. Kwahiyo hata wakati wa kufanya muraja'a ukiwa nyumbani ni vizuri ukamtafuta mtu wa kukusikiliza hasahasa kabla hujawa mzoefu.

Chapa gani utumie wakati wa kuhifadhi

Ni lazima utumie aina moja ya msahafu (chapa ya aina moja ya msahafu) wakati unapohifadhi quran.

Chapa za misahafu zinatofautiana mfano aya fulani inaweza ikawa katikati ya ukurasa katika chapa hii lakini ukichukua chapa nyingine aya hiyo hiyo ipo juu ya ukurasa. Sasa wakati unapohifadhi ukitumia leo chapa hii na kesho chapa nyingine unakuwa unajichanganya kuhusu mpangilio wa aya. Hii ni kwasababu wakati unapohifadhi yaani wakati unarudia aya mara nyingi pia macho yanakuwa yanahifadhi mpangilio wa aya.

Mtu aliyehifadhi quran anakuwa anajua aya fulani ipo juu au katikati au chini ya ukurasa hivyo ni muhimu sana kutumia chapa ya aina moja ya msahafu kama chapa maarufu ya King Fahd (Chapa ya Saudia)

Nini ufanye mara baada ya kumaliza kuhifadhi quran?

- Baada ya kumaliza kuhifadhi quran yote ule mwaka wa mwanzo baada ya kuhitimisha ni muhimu kufanya muraja'a mzito kwani ukizembea kipindi hiko quran hupotea haraka katika kifua chako. Ni vizuri katika mwaka huo kwa uchache kabisa uhitimishe quran ndani ya wiki moja yaani kila siku ufanye muraja'a japo juzuu 5 ikiwa utaweza. Kipindi hiki baada ya kumaliza kuhifadhi quran yote ndio kipindi cha kukusanya juzuu zote 30, hivyo usijisikie vibaya na sheitwan asije kukuchezea endapo utapata ugumu kidogo katika kuzikusanya juzuu zote. Huenda ukapata ugumu kidogo ukirudia juzuu za mwanzo kama vile juzuu ya 6 na kuendelea. Hii ni kwasababu aya nyingi katika quran zinafanana na maneno ni yaleyale hivyo baada ya kumaliza kuhifadhi quran yote ulimi unakuwa bado haujazoea kutofautisha na kukusanya aya zote kwa pamoja.

- Kuna watu wa sampuli mbili hapa, kuna yule ambaye akimaliza tu kuhifadhi juzuu zote 30 hapohapo anaweza hata kushiriki mashindano ya quran na akafanya vizuri. Hii ni kwasababu alikuwa akifanya muraja'a mara kwa mara toka kipindi bado anaendelea kuhifadhi quran.

  Na kuna yule ambaye akimaliza kuhifadhi juzuu zote 30, hifdhi yake inakuwa bado dhaifu na akifanya muraja'a juzuu alizohifadhi zamani anapata ugumu. Kwahiyo humchukua takribani miezi 6 mpaka mwaka kuziweka vizuri juzuu zote 30 katika kifua chake. Huyu ni yule ambaye alikuwa akizembea au alikuwa hafanyi muraja'a mara kwa mara kabla ya kumaliza kuhifadhi msahafu wote.

  Kwa hali zote mbili hapo juu, ni vizuri kufanya muraja'a mzito baada ya kumaliza juzuu zote 30 ili zipate kukita zaidi katika kifua.

MURAJA'A NA AINA ZAKE

Kumbuka kitu kimoja, usihifadhi quran bila ya kufanya muraja'a. Ili hifdhi yako iwe kali au yenye nguvu lazima ufanye muraja'a mara kwa mara.

Anasema Allah aliyetukuka katika kitabu chake

"Allah ameteremsha maneno mazuri kabisa, kitabu chenye kufanana na kurudiwa mara kwa mara" (Az-zumar: 23)

Pia amesema Mtume (swalla Allahu alaihi wasallam)

"Ichungeni sana quran, naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mkononi mwake kwa hakika ni nyepesi sana kutoroka kutoka vifuani mwa watu kuliko ngamia kutoka katika kamba yake" (Bukhariy: 5033 na Muslim: 790)

Tofauti kati ya juzuu darsa na muraja'a

Juzuu darsa ni marejeo katika juzuu au sehemu ya juzuu ambayo mtu amehifadhi hivi karibuni. Kwa upande mwingine, Muraja'a ni kufanya marejeo ya juzuu zote za nyuma ambazo mtu amehifadhi kwa kiwango maalum.

Baadhi ya Markaz za tahfidh hawana kipindi cha juzuu darsa yaani huchanganya pamoja na muraja'a na kuita jina moja tu yaani Muraja'a (Marejeo). Lakini baadhi ya Markaz hutofautisha yaani juzuu darsa muda wake na muraja'a muda wake.

Hapa tutaeleza namna ya kufanya marejeo kwa ujumla wake (yaani Muraja'a kwa ujumla wake).

AINA ZA MURAJA'A

Zifuatazo ni aina za muraja'a kutokana na utaratibu tulioutaja

(i) Muraja'a wa kila siku
(ii) Muraja'a baada ya kumaliza juzuu 5
(iii) Muraja'a baada ya kumaliza juzuu zote 30 (baada ya kumaliza msahafu wote)

(I) MURAJA'A WA KILA SIKU

- Mfano, jana ulihifadhi ukurasa wa kwanza katika suratul-mulku. Leo kabla ya kuanza kuhifadhi ukurasa mwingine soma ukurasa wa jana mara 3 kwa kuangalia kisha soma mara 2 bila kuangalia ili ukurasa wa jana uendelee kukita katika kifua chako kabla ya kuanza ukurasa mpya. Fanya hivi katika kile kipindi cha hifdhul quran katika ratiba ya madrasa kisha ndio unaendelea kuhifadhi ukurasa mwingine mpya. Hilo ni mosi, kuanza kufanya muraja'a mfupi kabla kuendelea kuhifadhi ukurasa mwingine mpya.
- Pili, katika kile kipindi cha juzuu darsa na muraja'a utafanya marejeo kwa kutumia utaratibu ufuatao:

Kwa madrasa za kutwa

(1) Mwanafunzi mwenye uwezo wa chini kila siku atafanya muraja'a karatasi 1 na mwanafunzi mwenye uwezo wa kati kila siku atafanya muraja'a karatasi 2.

(2) Mwanafunzi mwenye uwezo wa juu kila siku atafanya muraja'a karatasi 3.

Kwa madrasa za bweni

(1) Mwanafunzi mwenye uwezo wa chini kila siku atafanya muraja'a karatasi 2 na mwanafunzi mwenye uwezo wa kati kila siku atafanya muraja'a karatasi 3.

(2) Mwanafunzi mwenye uwezo wa juu kila siku atafanya muraja'a karatasi 5.
Ni vizuri mwanafunzi asizidishe zaidi ya kiwango hiko kwa siku isipokuwa kama muda bado anao atumie muda huo kurudia mara nyingi ili hifdhi yake izidi kuwa kali zaidi.

Nini ufanye ili uweze kufanya muraja'a karatasi nyingi zikiwa vizuri?

- Soma karatasi 2 zote kwa pamoja mara mbili au mara tatu kwa kuangalia kisha baada ya hapo soma mara 2 bila kuangalia, utaona unapata wepesi sana na unasoma bila kukwama.

- Hivi ndio kufanya muraja'a kwa mtu ambaye bado hajawa mzoefu na quran bado haijakita sana katika kifua chake.

- Kwa mtu ambaye anafanya muraja'a kila siku karatasi 5, atagawa karatasi 3 anafuata utaratibu huo kisha karatasi 2 anafuata utaratibu huohuo yaani anasoma mara mbili au mara tatu kwa kuangalia kisha ndio anasoma mara mbili bila ya kuangalia.

(II) MURAJA'A BAADA YA KILA JUZUU 5

Kama tulivyoeleza hapo awali, kila baada ya kumaliza juzuu 5 mwanafunzi atasimamishwa kuhifadhi na ustadh wake kwa siku 10 ili afanye muraja'a wa jumla ulio mzito kwa hizo juzuu alizozihifadhi.

Mwanafunzi akizitumia vizuri hizi siku 10 basi juzuu alizozihifadhi zinakuwa zimekaa vizuri na anaweza hata kushiriki mashindano ya quran hizo juzuu 5 na akafanya vizuri.

Baada ya kumaliza juzuu 5, mwanafunzi anakuwa sio wa uwezo wa chini tena. Mwanafunzi huyu anakuwa ni mwenye uwezo wa kati au uwezo wa juu.

Kwa madrasa za kutwa

(1) Kwa mwanafunzi mwenye uwezo wa kati, kila siku atafanya muraja'a karatasi 5. Hivyo juzuu 1 ataimaliza kwa siku 2 kwahiyo juzuu zote 5 atakuwa amezifanyia muraja'a ndani ya siku 10.

Kwakuwa kipindi hiki ana muda mrefu wa kufanya muraja'a kwasababu amesimamishwa kuhifadhi basi huenda akapata muda wa kurejea tena mara ya pili ndani ya hizo siku 10. Kuna Jumamosi na Jumapili ambazo zina muda mrefu kwa madrasa za kutwa hivyo ustadh wake ndio atamruhusu kuzidisha zaidi ya kiwango hiko kwa baadhi ya siku ikiwa ataona analeta kazi vizuri na muda bado anao wa kutosha.

Muraja'a wa hizi karatasi 5 kwa siku itakuwa kama ifuatavyo; atasoma karatasi zote 5 kwa pamoja mara mbili kwa kuangalia kisha atasoma mara mbili bila kuangalia.

(2) Mwanafunzi mwenye uwezo wa juu, kila siku atafanya muraja'a juzuu moja (karatasi 10).

Atasoma karatasi 5 zote kwa pamoja mara mbili kwa kuangalia kisha atasoma mara moja au mara mbili bila kuangalia. Baada ya hapo, atasoma karatasi 5 nyingine mara mbili kwa kuangalia kisha atasoma mara moja au mara mbili bila kuangalia.

Kwa madrasa za bweni

(1) Mwanafunzi mwenye uwezo wa kati kila siku atafanya muraja'a juzuu moja kwa utaratibu tulioelezea hapo awali.

(2) Mwanafunzi mwenye uwezo wa juu kila siku atafanya muraja'a juzuu mbili kama tulivyoelezea yaani kila karatasi 5 anasoma zote kwa pamoja kwa kuangalia mara mbili kisha anasoma mara moja au mara mbili bila kuangalia.

(III) MURAJA'A BAADA YA KUMALIZA JUZUU ZOTE 30 (MSAHAFU MZIMA)

Kwa madrasa za kutwa

- Baada ya kumaliza kuhifadhi juzuu zote 30, mwanafunzi ataanza na muraja'a wa juzuu mbili kila siku, kwahiyo ndani ya siku 15 atakuwa ashafanya muraja'a msahafu mzima. Baada ya miezi miwili kila siku atakuwa anafanya muraja'a juzuu tatu. Kutokea hapo, baada ya miezi mitatu mingine atakuwa anafanya muraja'a juzuu 5 yaani juzuu 3 anasikilizwa madrasa na juzuu 2 anaenda kufanya muraja'a mwenyewe akiwa nyumbani. Hii ni kwasababu muda wa madrasa ni mfinyu lakini ustadh wake atakuwa anamtolea mapande juzuu tofauti tofauti ili kuijenga hifdhi yake.
- Mwanafunzi mwenyewe akiamua kuongeza muraja'a zaidi ya juzuu 5 kwa siku itakuwa bora zaidi endapo atatumia muda wake wa ziada hata akiwa nyumbani.

Muhimu kuzingatia

Mwanafunzi akishajiona kuwa quran imeshamkaa vizuri kuanzia hapo atakuwa anafanya muraja'a bila kuangalia moja kwa moja ikiwa ni tofauti na utaratibu wa muraja'a tuliouelezea hapo awali.

Kwa madrasa za bweni

- Mwanafunzi huyu baada ya kumaliza kuhifadhi juzuu zote 30, ataanza kufanya muraja'a juzuu 3 kila siku kwahiyo ndani ya siku 10 atakuwa ameshafanya muraja'a msahafu mzima. Baada ya miezi miwili mwanafunzi huyu ataanza kufanya muraja'a juzuu 5 kila siku kwahiyo ndani ya siku 6 atakuwa ameshafanya muraja'a juzuu zote 30 (msahafu mzima).

- Siku mwanafunzi akipata muda wa kutosha, afanye muraja'a hata juzuu 10 kwa siku, kuna vitu atapata akifanya muraja'a juzuu nyingi. Quran ni kitabu cha ajabu kwani kila siku ukifanya muraja'a kuna tofauti mpya ya aya mbalimbali utaiona ambayo hukuiona kabla na hasahasa kabla hujawa mzoefu.

Muraja'a baada ya quran kukita katika kifua chako

Baada ya kumaliza kuhifadhi msahafu wote, kuna wakati ukishafanya muraja'a mzito kwa muda mrefu utajiona kuwa hifdhi yako tayari ishakaa sawa na kuwa kali. Baada ya hapo unaweza hata kupunguza kiwango cha muraja'a kwa siku na wala haina shida. Mfano, kila siku unaweza kufanya muraja'a juzuu moja au hata siku moja au siku mbili zikakupita hujafanya muraja'a bado qur-an haitoki katika kifua chako kwakuwa ulifanya jitihada kubwa mwanzoni na quran ikakita katika kifua chako. Hivyo tunasisitiza kufanya muraja'a mzito punde tu baada ya kumaliza kuhifadhi quran yote kama tulivyoeleza.

Mambo ya ziada ambayo huongeza ubora katika hifdhi ya mtu

(1) Kufanya muraja'a vizuri na kuswalisha taraweh kila mwaka hufanya quran izidi kukita katika kifua chako.

(2) Kusoma nusu juzuu au juzuu moja katika swala za usiku kwani baada ya kuamka usiku mwili unakuwa umechangamka na akili imetulia.
Anasema Allah aliyetukuka katika kitabu chake

"Hakika kuamka usiku kunaafikiana zaidi na moyo na maneno yake yanatua zaidi" **(Muzzammil: 6)**

"Kwani hakika mchana una shughuli nyingi" **(Muzzamil: 7)**

(3) Sura yoyote au sehemu yoyote ya quran ambayo mtu ataisikiliza mara kwa mara katika audio hufanya mtu apate wepesi mno katika kuihifadhi sura hiyo au sehemu hiyo ya quran. Hivyo ni vizuri ukasikiliza quran katika audio mara kwa mara hata baada ya kumaliza kuhifadhi quran yote kwa kutumia msomaji yeyote mashuhuri unayempenda.
Hii ni njia ya kusikiliza, kwa upande mwingine, sura yoyote au sehemu yoyote ya qur-an ambayo mtu ataisikia msikitini imamu akiisoma mara kwa mara (mfano: kuanzia "Lau anzalnaa" mpaka mwisho) hufanya mtu apate wepesi katika kuhifadhi sura hiyo au sehemu hiyo ya quran.

(4) Muhimu pia kwa anayehifadhi quran kujifunza lugha ya kiarabu kwani inasaidia kwa kiasi fulani katika kukumbuka aya, mfano mpangilio wa aya zinazoelezea kisa fulani. Ndio maana waliohifadhi quran wengi duniani wanajua lugha ya kiarabu.
Hivyo tunashauri katika ile ratiba ya madrasa ambayo siku moja kwa wiki ni siku ya kusoma vitabu vingine vya dini iwekwe lugha ya kiarabu katika moja ya vipindi kwa siku hiyo.

(5) Pia ni vizuri kwa anayehifadhi quran kujua tafsiri za aya anazozihifadhi kwani husaidia pia katika kukumbuka. Baadhi ya wanafunzi huwa na **msahafu wa tafsiri** kwa ajili ya kuangalia tarjama za aya.

Mfano, mwanafunzi ameanza kuhifadhi ukurasa mmoja kabla ya kuendelea kuhifadhi ukurasa mwingine anachukua msahafu wa tafsiri ya kiswahili anasoma tafsiri ya ukurasa aliohifadhi kisha ndio anaendelea kuhifadhi ukurasa mwingine.
Kufanya hivi ndio lengo la quran litafikiwa kwani lengo la quran ni kuifanyia kazi mafundisho yake na ili uweze kuifanyia kazi lazima uelewe maana yake.

Anasema Allah aliyetukuka katika kitabu chake

"Kitabu tumekuteremshia wewe, chenye Baraka ili wazingatie aya zake na wakumbuke (wawaidhike) wenye akili" **(Swaad: 29)**

Zama hizi tuna baadhi ya vijana waliohifadhi quran ambao tabia zao sio nzuri. Hii ni kwasababu hawafahamu maana ya maneno mazito waliyoyabeba kwahiyo wanaghafilika katika kuyafanyia kazi. Watu hawa waliobeba maneno ya Allah kisha hawayafanyii kazi, Allah kawapigia mfano mbaya sana ni mfano wa punda anayebeba vitabu vikubwa vikubwa lakini havimnufaishi na chochote. Kwahiyo ni muhimu kujua tafsiri ya quran ambayo mtu anaihifadhi. Tunamuomba Allah tawfiq na atupambe tabia zetu kwa mujibu wa mafundisho ya quran.